**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**
**HALIMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA**
**SHULE YA SEKONDARI WOTTA**

**NAMBA ZA SIMU:**
**MKUU WA SHULE: 0767002942**
**MAKAMU: 0765066091**
**MTAALUMA: 0788583668**

Mzazi /Mlezi wa mwanafunzi ……………………………………
S.L.P ………………………………………………………………..
……………………….

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO (V) KATIKA SHULE YA SEKONDARI WOTTA HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA MKOA WA DODOMA MWAKA ………………….**

**1.0. UTANGULIZI.**

Ninafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya Sekondari WOTTA mwaka ………………… kwa tahasusi ya__________ ( **HKL na EGM ).**

Shule ipo Mkoa wa **Dodoma**,Wilaya ya **Mpwapwa**, kata ya **Wotta**, umbali wa kilomita 77 kutoka Mpwapwa mjini kuelekea **Kibakwe -Wotta**.Usafiri wa basi kutoka Mpwapwa mjini unapatikana katika kituo cha mabasi Mpwapwa mjini na nauli ni shilingi 20,000/=(Mpwapwa – Kibakwe Tsh 5,000 na Kibakwe – Wotta Tsh 15,000/=) tu.

Muhula wa masomo unaanza tarehe ……………….. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti tarehe **……………….** na mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………….. Mara utakapofika shuleni unatakiwa kuripoti kwa makamu Mkuu wa Shule ambaye atakupokea na kukusajili rasmi.

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.0.1 SARE ZASHULE:**

**i. WAVULANA**

Suruali 2 nyeusi kitambaa kizito zenye turnup/mkunjo wenye upana wa sentimeta 16, koti jeusi la suti vifungo viwili, sweta rangi ya ugoro(itapatikana maduka yaliyopo karibu na shule), Mashati mawili (2) meupe ya mikono mirefu yenye nembo ya Shule yatapatikana maduka yaliyo karibu na shule, fulana ya rangi ya blue (form six) ambayo itapatikana maduka yaliyopo karibu na Shule, tai ndefu itapatikana maduka yaliyopo karibu na shule, Viatu vyeusi vya kubrash na kiwi jozi mbili vya kufunga na kamba vyenye kisigino kifupi na soksi nyeusi ndefu jozi mbili zisizo na maandishi, mkanda mweusi, suruali ya dark blue pamoja na track suit ya

kijivu aina ya adidasi itapatikana maduka yaliyopo karibu na Shule pamoja na Puluneki nyeupe nzito.

ii. **WASICHANA**

Sketi 2 nyeusi kitambaa kizito zenye marinda makubwa yasiyozidi nane ndefu zinazo karibia kiwiko cha mguu.,koti jeusi la suti kifungo kimoja, sweta rangi ya ugoro, Mashati mawili (2) meupe ya mikono mirefu, fulana ya rangi ya blue (form six) na Tai ndefu nyeusi, Viatu vyeusi jozi mbili vya kufunga kwa kamba visivyo na mchongoko, soksi nyeupe ndefu jozi mbili zisizo na maandishi, sketi moja ndefu dark blue yenye marinda ya kawaida, track suit ya kijivu na hijabu nyeupe (kwa Waislamu).Puluneki nyeupe nzito.

**NB: UNIFOMU ZA SHULE ZITASHONWA NA FUNDI ALIYETEULIWA NA SHULE AMBAYE ANAPATIKANA KWA NAMBA: 0719716545.**

### 2.0.2. VAZI LA HIJABU

Pamoja na maelekezo ya sare nyingine za Shule hapo juu vazi la Hijabu linaruhusiwa kwa kuzingatia

i. Hijabu nyeupe kwa ajili ya darasani.
ii. Hijabu ya rangi ya maziwa kwa ajili ya shughuli nyi gine za nje.

### 2.0.3. SARE BAADA YA MASOMO

Baada ya masomo Wanafunzi wanatakiwa kuvaa sare maalumu(Shamba dress) ambapo wavulana watatakiwa kuvaa suruali ya dark blue ambayo mshono wake utakuwa sawa na maelekezo ya sare za darasani na fulana ya blue yenye nembo ya Shule.

Kwa Wasichana watavaa gauni la dark blue mbili zenye marinda ya kawaida na ndefu zinazofikia kifundo cha miguu.

### 2.0. 4. SARE ZA MICHEZO

Bukta na fulana ya bluu ya Taifa Stars kwa Wavulana,Bukta na fulana nyeupe ya Taifa Stars na jozi moja ya raba nyeupe isiyo na kisigino au soli ndefu.

### 2.0.5 MAHITAJI MENGINE AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI:

1. Shuka mbili za rangi ya Bluu, blanketi 1 na chandarua,
2. Godoro futi $2^1/_2$.lililo imara.
3. Jembe 1 lenye mpini na kwanja
4. Sabuni ya maji lita 5
5. Ndoo 2 za lita 10 (moja kwa matumizi binafsi na moja matumizi ya shule)
6. Mfagio 1 (soft bloom), drier 1 (rabber squizer), hard bloom1 na ufagio wa nje (chelewa).
7. Reki moja.
8. Brashi ya chooni
9. Dawa ya chooni aina ya Aro 2
10. vyombo vya chakula (sahani, kijiko, kikombe )
11. Picha nne(Pasport size)
12. Tochi ya betri za kawaida kwa ajili ya matumizi ya dharula.

### 2.0.6. VIFAA VINAVYOTAKIWA DARASANI.

1. Daftari kubwa 8 (Counter book-quire 3 au 4)
2. Mafaili saba(7) ya plastic kwa ajili ya kutunzia mitihani yako na mazoezi).
3. Kikokotozi (**scientific calculator kwa EGM**), Mkebe, rula, kalamu na penseli za kutosha.
4. Aje na karatasi(**rimu)** mbili(2) A4 aina ya rotatrim kwa ajili ya mitihani na mazoezi ya mara kwa mara.
5. Wasilisha nakala ya cheti cha kuzaliwa, leaving certificate pamoja na result slip kwa matumizi ya shule.

**Vifaa vinapatikana katika duka lililo jirani na shule kwa bei nafuu sana kuepuka usumbufu safarini.**

**3.0 . MICHANGO MBALIMBALI**

i. Michango inayotakiwa kulipwa na mzazi ni hii ifuatayo; Tshs. **5,000**/= kwa ajili ya tahadhali (haitarejeshwa),
ii. Tshs. **5,000**/= kwa ajili ya kitambulisho.
iii. Tshs. **5,000**/= kwa ajili ya nembo
iv. Tshs. **65,000**/= kwa ajili ya uendeshaji wa shule.

**Jumla ya michango ni Tshs 80,000/= tu.**

**NB. Michango hiyo yote ilipwe kupitia benki ya NMB AC/NA. 50401100038 JINA LA AKAUNTI: WOTTA SECONDARY REVENUE COLLECTION. Tawi lolote.** ***Hatupokei fedha mkononi,mwanafunzi aje na risti ya benki (deposit slip)***

**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na.25 ya mwaka 1978 nakama ilivyorekebishwa kwa sheria na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo muhimu yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.mambo hayo ni pamoja na:

1. Heshima kwa viongozi, walimu, wafanyakazi wote, wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
2. Kushiriki au kuanzisha mgomo wa aina yoyote wala maandamano kinyume na sharia ya nchi ni kosa na hivyo utafukuzwa shule moja kwa moja.
3. Kumpiga Mwalimu au Mfanyakazi yeyote, mwananchi yoyote ni kosa.
4. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
5. Ni wajibu wako mwanafunzi Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, kutii kengele na Kuwahi kila mahali utakapohitajiwa na kwa wakati.
6. Kujua mipaka ya shule na kuzingatia maelekezo yote juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii. Kukosa kufanya hivyo adhabu kali itatolewa ikiwa ni **kurudishwa nyumbani na kujenga wigo**.
7. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
8. Niwajibu wako mwanafunzi Kuvaa sare ya shule wakati wote utakapokuwa shuleni. Kamwe nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa na iwapo utakiuka taratibu hizi adhabu kali itatolewa ikwa ni pamoja na kusimamishwa masomo.

9. Ni marufuku mwanafunzi kuvaa viatu vyenye kisigino kirefu, soli ndefu au pana wala kiatu kilichochongoka mbele, mkanda usio mweusi, mkanda wenye chuma/bakuli kubwa au mapambo mengine kama heleni, mikufu, bangili. Pia ni marufuku kufuga rasta, nywele ndefu, ndevu, kupaka kucha rangi, kupaka wanja, kupaka piko, kujichubua, kunyoa kipara. Atakayepatikana na makosa haya atarudishwa nyumbani na kumwita mzazi.
10. Huruhusiwi kuwasha moto wowote ndani ya bweni au kwenye mazingira ya shule na hata darasani. Pia ni marufuku mwanafunzi kuwasha moto jikoni. Adhabu kali zitachukuliwa dhidi yako.
11. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki simu, DVD, kamera, pasi ya umeme, mishumaa na silaha ya aina yoyote ikiwemo vilipuzi. Kukutwa na kosa hilo utafukuzwa shule kabisa na bila huruma.
12. Huruhusiwi kuvaa mavazi yaletayo aibu kama vile suruali/sketi ya kubana, fupi, mlegezo, wala nguo yoyote isiyo ya maadili.
13. Enndapo mwanafunzi utafanya uharibifu wowote ndani ya shule, utachukuliwa hatua kali ikiwemo kufukuzwa shule/ kusimamishwa na kulipa gharama za uharibifu huo.
14. Kila mwanafunzi ataheshimu tarehe ya kufungua na kufunga shule. Endapo atachelewa kufungua shule ataadhibiwa kwa kurejeshwa nyumbani na kumleta mzazi.
15. Mwanafunzi anawajibika kuheshimu Bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa, Mwenge wa Uhuru, fedha ya nchi,picha za VIongozi pamoja na alama zingine za Taifa.
16. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuishi kwa amani mahali popote na kuto kupiga wa kupigana, vurugu ya aina yoyote, kupiga kelele ya aina yoyote. Kufanya hayo yatasababisha ufukuzwe shule kabisa.
17. Ni marufuku mwanafunzi kuvuta bangi wala kukutwa na kilevi cha aina yoyote, kushiriki ulevi wa aina yoyote ama kuuza mdawa ya kulevya. Kufanya hivyo itakuwa kosa la jinai na itakupasa uvuliwe uanafunzi na kufikishwa kwenye vyombo vya sharia.
18. Mwanafunzi haruhusiwi kubaki bwenini wakati wa masomo bila kibali cha mwalimu mlezi wa bweni ama mwalimu wa zamu.
19. Mwanafunzi hataruhusiwa kumiliki pesa bwenini isipokuwa fedha ya matumizi ya mwezi husika. Fedha yote iwe kwenye akaunti ya mwanafunzi au itunzwe kwa mwalimu wa fedha na mwanafunzi utasaini makabidhiano hayo Kinyume na kanuni hizo hapo juu, adhabu kali zitachukuliwa dhidi yako.

**MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa,
2. Wizi wa aina yoyote.
3. Kutoa lugha ya matusi / lugha chafu.
4. Kugoma au kuhamasisha mgomo.
5. Kupigana au kupiga.
6. Utoro.
7. Uasherati, kubaka au kulawiti, mahusiano ya kimapenzi ya jinsia moja.
8. Kuoa ama kuolewa.
9. Kupata ujauzito, kusababisha mimba na kutoa mimba.
10. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria ya nchi;
11. Kutembelea majumba ya starehe, guest house au hostel ya wasichana.
12. Ulevi /Kutumia kileo au madawa ya kulevya ya aina yeyote na kwa jinsi yeyote.
13. Kudharau Bendera ya Taifa.
14. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule na 15.Kosa lolote la jinai.

16. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kijiua ama kunywa sumu;
17. Kukutwa na Kiripuzi cha aina yoyote.
18. Makosa mengne yafananayo na hayo hapo juu.

**ANGALIZO – ANGALIZO - ZINGATIO**

***1.*** **Simu ya mkononi, pasi ya umeme na hita, mshumaa, visu au silaha ya aina yoyote, shuleni na redio inayotumia umeme haviruhusiwi kabisa. Ukikamtwa utalipa faini ya uharibifu uliowahi tokea/ uliotokea, au kufukuzwa shule bila huruma.**
***2.*** **Nguo zingine za nyumbani haziruhusiwi kabisa.**

**KARIBU SANA WOTTA SEKONDARI**

**………………………..**
**ARTHUR KINUNDA.**
**MKUU WA SHULE.**

# FOMU YA KIAPO CHA MWANAFUNZI.

**MIMI MWANAFUNZI ________________________________ WA TAHASUSI YA NIMESOMA NA KUZIELEWA SHERIA NA KANUNI ZOTE ZA SHULE NA KWAMBA NINAKUBALIANA NA SHERIA NA KANUNI NA NITAZITII MUDA WOTE NIWAPO SHULENI. NA NINAAHIDI KUWA MZALENDO WAN CHI NA SHULE KWA UJUMLA. IWAPO NITAKIUKA SHERIA NA KANUNI MOJAWAPO YA HIZO NICHUKULIWE HATUA SITAHIKI ZA KINIDHAMU.**

**"MUNGU NISAIDIE."**

***Jina La Mwanafunzi*_____________________________ *Tahasusi ya*__________**

***Sahihi au Dole Gumba la mwanafunzi*________________**

***''KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI WOTTA''***

…………………………

**ARTHUR KINUNDA**
**MKUU WA SHULE**

# FOMU YA KIAPO CHA MZAZI/ MLEZI WA MWANAFUNZI.

**MIMI MZAZI/ MLEZI WA MWANAFUNZI _____________________________ NINAKIRI KUPOKEA FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI WOTTA YENYE KIAMBATA CHA SHERIA NA KANUNI ZA SHULE ZITAKAZO MUONGOZA MWANANGU KUISHI KWA AMANI NA UTULIVU MUDA WOTE AWAPO SHULENI. AIDHA MAKOSA YATAKAYOMSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI YAKINI NA IWAPO MWANAFUNZI HUYU ATAKIUKA SHERIA NA KANUNI ZA SHULE TARATIBU ZA KISHERIA ZICHUKULIWE NA SHULE DHIDI YAKE. NINAAHIDI KUSHIRIKIANA NA UONGOZI WA SHULE KULINDA NIDHAMU YA MWANAFUNZI HUYU.**

## "MUNGU ANISAIDIE."

***Jina La Mzazi/Mlezi*__________________*Sahih*________________**

…………………………

**MKUU WA SHULE**

# OFISI YA WAZIRI MKUU
## TAWALA ZA MIKOA NA SERILALI ZA MITAA
### SHULE YA SEKONDARI WOTTA
### S.L.P. 287MPWAPWA - DODOMA

**FOMU YA UCHUNGUZI WA AFYA**

**DAKTARI: ………………………………**

**HOSPITALI: …………………………….**

**S.L.P. …………………………………….**

**YAH: KUPIMWA AFYA YA MWANAFUNZI ………………………………………………**

**Tafadhali tunaomba umpime mwanafunzi aliyetajwa hapo juu kwa gharama za mzazi/mlezi wake na uthibitishe kama ataweza kumudu mazingira ya shule hii iliyo eneo la baridi kwa vipimo vifuatavyo:**

- **Urine analysis: ……………………………………………………………………………….**
- **Stool examination: …………………………………………………………………………..**
- **Syphilis test: ………………………………………………………………………………**
- **Blood count (Red and White): ………………………………………………………..**
- **Eye test: ……………………………………………………………………………………..**
- **T.B. Test: …………………………………………………………………………………**
- **Ear test: ……………………………………………………………………………………...**
- **Spleen test: ………………………………………………………………………………….**
- **Other abnormalities: ………………………………………………………………….**

**Nathibitisha kuwa mwanafunzi mtajwa hapo juu ataweza/hataweza kumudu masomo ya sekondari.**

| | | |
|---|---|---|
| …………………………… | ………………………….. | ……………… |
| **JINA LA DAKTARI** | **SAHIHI NA MHURI** | **CHEO** |

**<u>TAFADHARI:</u>**

***mzazi/ mlezi hakikisha mwanafunzi anapimwa ili tujue afya yake na udhaifu wake ili tuweze kumpa huduma na uangalizi wa karibu katika kipindi chake cha masomo.***